**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, SLP 113, SHINYANGA
Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz
**Tovuti: www.shinyangadc.go.tz**

***Unapojibu tafadhali taja:***
Kumb.Na. SDC. C.4/7/I/66

24.05.2022

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kupitia Kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (UTUMISHI) anatangaza nafasi ya kazi kwa Wananchi wa Tanzania wenye şifa na ujuzi wa kujaza nafasi zifuatazo:-

1: **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 16)**

(a) **Sifa za Mwombaji:**

- Awe amehitimu Kidato cha Nne au Sita na Cheti cha Mafunzo (NTA LEVEL5) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi yaSanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) **Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III**

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo.-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano Mikuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

(c) **Ngazi ya Mshahara:**

Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

2: **Katibu Muhtasi Daraja la III (Nafasi 02)**

(a) **Sifa za muombaji**:

Awe amehitimu wa kidato cha IV amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu Mtihani wa Hatua ya Tatu. awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsofft Office, Internet, E-mail na Publisher.

**(b) Kazi na majukumu ya Katibu Mahtasi Daraja III**

Katibu Muhtasi atatekeleza majukumu yafuatayo.-

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaidia shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wakazi.

**(c) Ngazi ya Mshahara:**

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

## 3: MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE JUMLA

(i) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18-45,

(ii) Mwombaji aliyewahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa,

(iii) Barua ya mwombaji ioneshe anuani anayotumia kwa sasa Pamoja na namba za simu ikiambatana na:

a) Maelezo binafsi ya mwombaji (CV)

b) Nakala za vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali (Taaluma) kwa kuzingatia sifa tajwa hapo juu.

c) Nakala ya cheti cha kuzaliwa

d) Picha mbili (2) za Passport Size za hivi karibuni

**e) Kitambulisho au namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)**

(iv) Watakaochaguliwa kuhudhuria usaili (Shortlisted Candidates) watafahamishwa kupitia anuani na namba za simu walizotumia kwenye barua zao za maombi ya kazi,

(v) **Testimonials na Provisional results havitakubalika,**

(vi) Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na Mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya cheti,

(vii) Nakala zote za vyeti vya Shule, Chuo, kitambulisho cha Taifa (NIDA), na cheti cha kuzaliwa vithibitishwe na Wakili yeyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa au Mahakama.

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifutayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya Shinyanga,**
**S. L. P 113,**
**SHINYANGA.**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06 Juni, 2022 saa tisa na nusu alasiri.**

**NB:** Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.shinyangadc.go.tz

Nice R. Munissy
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**



MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 113
SHINYANGA